KISWAHILI P2

Majibu

MWONGOZO WA KUSAHIHISHA KIDATO CHA NNE

1. UFAHAMU

a) **Mabadiliko yaliyohitajika**
- Mayatima kunyanyaswa kwa kunyang'anywa pesa.
- Kufunga milango ya ofisi za umma
- Kuwepo kwa foleni ndefu za watu wanaosubiri kuhudumiwa katika ofisi za umma
- Wanaostahili kuwahudumia raia kutokuwepo ofisini ili kuwahudumia.
- Kutoa rushwa / mlungura ili kutimiziwa haki yako.
- Wananchi kunyang'anywa/kuhiniwa haki zao.
- Mapendeleo/ubaguzi katika uajiri, kuajiri watu kwa kuangalia uhusiano na kujuana.
  (hoja chanya au hasi zikubaliwe) hoja 6 x 1 = 6

b) **Salma hakuwa mgeni ofisini hapo kwa sababu zifuatazo:**
- Alipofika ofisini mazungumzo baina ya taipu na karani yalikatika ghafla kwani walimjua
- Haulizwi jina na mpiga taipu anapofika ofisini.
- Anapoulizwa kwa neno moja 'yupo' anajibiwa kwa kuambiwa kuwa ameondoka. Hamtaji mhusika.
- Mpiga taipu anamjibu akibabaika kwa sababu anamjua Salma ni nani. 4 x 1=4

c) Ziara za Salma Mbiju (kwa mamake) hazikuwa na lengo la kumjulia hali bali kumtaka mamake ampe msaada / pesa. 1x1=1

d) Samir, ambaye alikuwa mtoto mpendwa, hangetumiwa chochote na mamake seuze yeye? Wiki mbili zilizopita alikuwa amefika hapo na kupewa shilingi elfu tatu kwa hivyo hakutarajia kupewa chochote. 2x1=2

e) **Vinyume vya;**
i) kutahamaki – kutumia ; kusahau
ii) pangu pakavu –matajiri; wakwasi. 2x1=2

2. UFUPISHO ( ALAMA 15)

a)
- Mikopo hutumiwa na watu wengi ili kujiendeleza kiuchumi.
- Mikopo inakubalika kote ulimwenguni
- Serikali nyingi hurasimisha ardhi za wananchi ili kutumika kukopa kutoka kwenye taasisi rasmi.
- Watu wengi hupendelea mikopo isiyo rasmi.
- Haiwezekani kukopa kutoka kwenye taasisi rasmi bila kulipa deni.
- Wakopaji hutumia mali yao kama rehani wanapokopa.
- Dhamana husimama kama mbadala wa mkopo. ( zozote 5 x 1=5)

b) **Hatari**
- Hushindwa kusimamia biashara / miradi wanayoanzisha kwa mikopo.
- Hawa hukosa kupata pesa za kulipia madeni kwa kuhasirika.
- Baadhi huwekeza kwenye miradi isiyozalisha faida na kupoteza kila kitu.
- Wengine hutumia mikopo katika anasa na kufilisika.
- Mali iliyowekwa rehani huuzwa (hupigwa mnada)



**Suluhisho**
- Wakopaji wanafaa kushirikishwa katika namna bora za kutumia fedha za mkopo kwa ajili ya uwekezaji endelevu.
- Wanafaa kuelimishwa kuhusu mbinu za kulipa madeni ili waepuke kufilisika.
- Wakopaji wanastahili kutathminiwa kwa kina kabla ya mikopo yao kuidhinishwa.
- Mashirika yanweza kutoa mikopo kwa awamu ili kuwadhibiti wakopaji wabadhirifu.

Hoja za kuonyesha hatari 4 x 1=4
Hoja za kuonyesha suluhisho 4 x1

MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)

a)
i) vikwamizo
ii) Hutamkiwa kwenye ufizi / masine
iii) sauti sighuna
iv) sauti ghuna ½ x 4=2

b)
i) nguo
ii) temwa 2 x 1=2

c) sijawapa 2 x 1=2

d) Nyembe walizonunua kwenye maduka zimewasaidia kuzikata kucha. 1 x 1=1

e) Magombe haya na yale yalivuka jito hilo kwa utaratibu. 1x1=1

f)
i) **Adhabu** ilitolewa kwa mwanafunzi na mwalimu kwa kufanya **makosa** au **Makosa** ya mwanafunzi kwa mwalimu yalimfanya apewe **adhabu** au Mwalimu alimpa mwanafunzi **adhabu** baada ya kufanya makosa. ½ x 2=1
ii) Nguo zilizonunuliwa juzi ziliuzwa kwa bei ghali au Nguo **ambazo** zilinunuliwa juzi ziliuzwa kwa bei ghali. 1 x 1=1
iii) Fasihi ilizushwa na mapambano baina ya mwanadamu na mazingira. 1 x 1=1

g)
i) Nguo zilizoraruka zimeshonwa au Nguo **ambazo** ziliraruka zimeshonwa. 1 x 1=1
ii) **Ijapokuwa** nilienda kwake mapema sikufanikiwa kuonana naye au **Maadamu** umefika mapema tutaanza mkutano. 1 x 1=1
iii) Usalama ukiimarika watalii wengi watazuru humu au Angesoma kwa bidii, angepita vizuri. 1 x 1=1

h) Miti michache ilikatwa. 1 x 1=1

i) Miongoni mwa wanariadha wa Kenya kuna wanariadha hodari 1 x 3=3

j) kisu kinolewacho ndicho kipatacho. 1 x 1=1

k)
i) kwa tano –akisami /uakifishaji wa idadi
ii) kwa gari –kitumizi /kifaa
iii) kwa mchuzi –pamoja na 3x1=3

l) Kahindi alipanda matatu nambari **saba**, kisha akamuuliza **dereva**, **"Gari** hili litanifikisha **Ukunda?"**
Kahindi – ½, saba, dereva, - ½ , " " - ½ , Gari – ½, Ukunda – ½ , ? – ½- ½ x 6=3

m) kupeka 1x1 =1
n) Sisi si wanafunzi 2 x 1=2
o) fiche, shaka. 2x1=2
p) Dereva yeyote atakayeendesha gari kwa kasi atapoteza kazi yake. (kadiria) 2x1=2
q) Viongozi fisadi watakuwa wakifishwa mahakamani. 2x1=2
r) yambwa tendewa/ kitondo –aliwanunulia
- yambwa tendwa/ kipozi –zawadi nzuri
- yambwa ala /kitumizi–shilingi elfu kumi 3x1=3
s) Shuleni mwetu mna majengo mapya. (nomino)
Mashindano ya kandanda yanafanyika shuleni. (kielezi) 2x1=2
t) Ukiwa mwenye bidii utapata fanikio maishani. 1x1 =1
u) Sentensi agizi
v) Kiti kilibebwa na seremala. 1x1 =1
w) Watoto walipana chakula 1x1 =1

3. **ISIMUJAMII (alama 10)**

a) Matumizi ya sentensi ndefu. Sentensi ya kwanza ina zaidi ya maneno 30.
- Matumizi ya msamiati maalum. "mswada, bunge"
- Vifungu vya sheria vinarejelewa. "kifungu cha 4…"
- Matumizi ya lugha sanifu. "sentensi ya kwanza ina lugha sanifu"
- Matumizi ya lugha kavu. "lugha inayotumiwa haina mapambo"
- Matumizi ya lugha ya heshima. "sheria za bunge hili tukufu…"
- Kuchanganya ndimi. "kufikia the one third rule…"
- Lugha ya kuibua utangamano. "ndugu zangu" (zozote mbili x1=2)

b) Matumizi ya uradidi/urudiaji. "mheshimiwa spika"
- Matumizi ya viziada lugha au ishara za mwili au uso
- Kutajwa kwa wahusika kwa majina. " Mheshimiwa Tunu"
- Wabunge kukatizana kalima.
- Matumizi ya lugha ya mzaha na kukejeliana.
- Lugha ya maswali na majibu
- Matumizi ya utohozi. "spika, bajeti"
- Matumizi ya lugha amrishi hasa na spika. "Mheshimiwa… keti!"
- Mtindo maalum wa kuanzisha na kuendeleza mjadala. " Mheshimiwa Bwana Spika"
- Lugha ya kushawishi. "ndugu zangu waheshimiwa naomba"

**(zozote tano za kwanza 5x1=5)**

TANBIHI: Kila sifa iandamane na mfano au maelezo.
Sifa bila mfano, alama nusu, mfano bila sifa sufuri.

Tamu sana! Very sweet! Very nutritious! Onja ujionee! Nunua. Nunua leo. Usikose mummy. Mchukulie mtoto. Fifty na Fifty! Hamsa. Fifty. Bure kwa bure! Bei ya starehe! Burudika.

a) Sajili ya biashara/ sokoni:Anasema nunua leo (alama 1)

b) Eleza sifa nne za sajili hii kwa kurejelea kifungu. (alama 4)
- Lugha ya kuvutia hutumiwa, bure kwa bure ili kuvutia wateja.
- Lugha shawishi mno hutumiwa, mfano bei ya starehe sana/ usikose mummy ili kuwavutia wanunuzi.



- Kuna matumizi ya takiriri nunua, nunua leo
- Kuchanganya ndimi, very sweet ili kuvutia wateja wengi.
- Huwa na ucheshi na porojo ili kuwavutia wateja. Mfano, bure kwa bure
- Lugha nyepesi hutumika ili kuwasilisha. Bei ya starehe
- Ubora wa bidhaa husisitizwa, ili kuwavutia wateja. Tamu sana
- Kuna upigaji chuku mwingi ili kuwavutia wateja. Mfano bure kwa bure.
- Sentensi fupi fupi hutumika kurahisisha mawasiliano. Mfano nunua, nunua leo.
- Lugha ya mafumbo-fifty na fifty (ni mia)

Mwanafunzi akitoa hoja kisha akose kusema **ili, au akose kutoa sababu, alama zake ni nunge.**